

KUISHI
BILA ZINAA
(Living without fornication)
DR. CHARLES KABIGUMILA

# KUISHI BILA ZINAA

## (Living without fornication)

# UTANGULIZI & SHUKRANI.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali cha kuandika kitabu hiki cha **kuishi bila zinaa**. Nimeandika kitabu hiki kwasababu kizazi hiki tulichopo Bwana Yesu mwenyewe alikiita kizazi cha zinaa *(Marko 8:38)* na hakuna mtu anayepinga kuwa tupo kwenye kizazi ambacho zinaa imekuwa ni janga la dunia. Ukweli ni kwamba kuna utofauti mkubwa wa zama za kale na sasa kwa mfanao zamani hakukuwa na teknolojia ya kurekodi video ya ngono na kuiweka mtandaoni ili watu watazame lakini zama hizi kwasababu ya kukua kwa teknolojia wamekusogezea zinaa karibu yako zaidi kupitia simu, kompyuta au Televisheni yako.

Kabla sijaokoka niliishi katika vifungo vya uzinzi na Mungu alinisaidia kutoka kwenye vifungo hivi na ndiomaana leo nina shauku kubwa ya kutaka vijana na wote wanaoishi katika dhambi hii waishinde kwani  zinaa ni adui mkubwa sana wa ndoa na maisha ya kusudi. ***Inawezekana kuishi bila zinaa*.**

Hali kadhalika ninamshukuru Baba yangu wa kiroho ***Bish.Dickson Kabigumila*** kwa malezi mazuri ya kiroho kwani niliokoka mikononi mwake akanisaidia kuzishinda dhambi za uzinzi na kwa malezi yake hadi kufikia uwezo huu wa kuandika kitabu.

Hiki sio kitabu cha kawaida kwako, haya yaliyoandikwa ni UWEZESHO wa kukusaidia wewe msomaji kuishinda jumla zinaa.

**© 2021 Charles Claudio Mashili**

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili, kudurufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi, na ukiukwaji wa taratibu hii unaweza kupelekea mashitaka toka kwa waandaaji wa kazi hii.

PST.CHARLES KABIGUMILA

Mwanza, Tanzania. East Africa

SIMU:+255746192605/

+255676092605

BARUAPEPE:Charlesmashili11@gmail.com

TOVUTI: www.divinefamily.co.tz

Email: charleskabigumila@gmail.com

FB & YOUTUBE: Dr.Charles Kabigumila tb

# YALIYOMO.


**1.KWANINI TUIKEMEE SANA ZINAA...............(7)**

**2.ZINAA NI NINI HASA?!..............................(13)**

**3.NINI KINAMFANYA MTU AZINI..................(20)**

**4.HATUA 5 KABLA YA KUZINI.......................(63)**

**5.ZINAA INAMFANYANINI MTU....................(69)**

**6.NATOKAJE KWENYE ZINAA.......................(93)**

**7.KUTENGA WAZINZI MAKANISANI.............(93)**

**8.JINSI NILIVYOISHINDA ZINAA................(108)**

# 1.0 KWANINI TUIKEMEE SANA ZINAA?!

## 1.1 Tunaishi katika kizazi cha Uzinzi.

Hatuwezi kuacha kuongelea dhambi za zinaa kwasababu hiki ni kizazi ambacho Bwana Yesu mwenyewe alikiita kizazi cha zinaa. Inaonekana kuna maisha ambayo Yesu mwenyewe aliyashangaa sana mpaka akaona akipe ‘lebel’ kizazi hiki kuwa uzinzi na uasherati ndio vimeshamiri mno mno. Na baada ya kusoma kitabu hiki utagundua ni kwa umuhimu gani imewapasa watu kuepuka dhambi inayoitwa zinaa.

Bwana Yesu katika kitabu cha Marko utaona ni kwa namna gani yeye pamoja na malaika watamuonea haya mtu ambaye atamuonea haya

Bwana Yesu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi;

***Marko 8:38***

***[38]Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.***

(Soma pia, Mathayo 12:39)

Maana ya haya maneno ni kwamba Yesu anajaribu kutuambia kuwa hiki ni kizazi cha dhambi ila hasa hasa ni dhambi ya uzinzi. Uzinzi aliona aupe uzito sawa na dhambi zingine zote kwa ujumla, inamaana kama ni kwa asilimia alisema uzinzi ni 50% na dhambi zingine zote akazipa 50%

Ndiomaana utakubaliana namimi kuwa kila eneo sasa uzinzi umetapakaa, iwe ni kwenye maeneo yetu ya kazi bado utakuta watu wanashawishika kutoa rushwa ya ngono ili wapewe kazi, kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii zinaa inapewa promo kwa kasi sana kupitia nyimbo, filamu, matangazo n.k

## 1.2 Zinaa ni dhambi pekee inayotakiwa kukimbiwa.

Zinaa ni dhambi ambayo ni tofauti na zingine, zinaa inatakiwa kukimbiwa na sio kufanyiwa maombi. Imeandikwa ikimbieni zinaa, hii inaonyesha ni kana kwamba dhambi ya zinaa ina miguu ya kuwakimbiza watu.

***1 Wakorintho 6:18***

***[18]Ikimbieni zinaa.(.....)***

Mfano wa kijana ambaye alikimbia alipoona ataanguka katika uzinzi ni Yusufu kutoka kwenye mikono ya mke wa Potifa ***(Mwanzo 39:12),*** maandiko yanasema alikimbia akiacha nguo yake mikononi kwa mwanamke, yaani alikubali kubaki uchi kuliko kuzini. Kuna kijana mmoja nahitaji kuongea na wewe juu ya hio tabia uliyonayo ya kutembeleana magetoni ukidai kuwa unajuamini. Hii dhambi huwa haina mbabe, usiruhusu kabisa majaribu ya aina hiyo, ni bora ukaikimbia zinaa kuliko kuilea, zinaa huwa haimchekei mtu.

## 1.3 Zinaa ni chanzo kikubwa cha kumkosa Mungu na mapenzi yake.

Zinaa ni njia nzuri ya Kumkosa Mungu, Watu wengi wamepoteza mahusiano yao na Mungu kwasababu ya zinaa, ni rahisi sana kufurahia kitendo cha dakika 15 ila baada ya hapo mtu akaishi na majuto mwaka mzima. Kijana Yusufu aliijua siri hii mapema hivyo pale alipoletewa fursa ya kulala na mke wa mwenye nyumba alimjibu kuwa afanyeje dhambi ya zinaa amkose Mungu?! Hii haijaandikwa kuwa amkosee Mungu, hapana ni AMKOSE Mungu, maana yake ni kwamba Mungu anakuwa hapatikani kwako jumla kama ukiwa mzinzi na ndiomaana anauita huu kuwa ni ubaya mkubwa.

***Mwanzo 39:9***

***[9]Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu cho chote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa NIMKOSE Mungu?***

Kuepukana na zinaa ni njia ya kuyatimiza mapenzi ya Mungu, kwahio kama mtu akiamua kuishi ndani ya zinaa anakuwa ameamua kuyakataa mapenzi ya Mungu.

*1 Wathesalonike 4:3*

*[3]Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati;*

# 2.0 ZINAA NI NINI HASA?!

Zinaitwa dhambi za zinaa kwasababu ni nyingi, yapo matendo kadhaa ambayo ukiyafanya moja kwa moja wewe unakuwa mhusika rasmi katika huu mfumo wa zinaa unaopeleka watu kuzimu kwa haraka sana.

## 2.1 ZINAA NI KUSHIRIKI TENDO LA NDOA NJE YA NDOA (UZINZI & UASHERATI).

•Uzinzi ni kitendo cha kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa na Uasherati ni kufanya tendo la ndoa ilihali haujaingia kwenye ndoa. Biblia inasema kila mtu atakayemwacha mkewe isipokuwa kwa habari ya UASHERATI anamfanya kuwa mzinzi na atakayemwoa pia atakuwa mzinzi ***(Mathayo 5:32).*** Kumbe mwanandoa naye anaweza kuwa muasherati ikiwa atafanya na watu wasio katika

ndoa.  Hapa ndipo utakuta mama mzima na ndoa yake analala na KIJANA WA CHUO, huu ni uasherati.

## 2.2 ZINAA NI KUFANYA TENDO LA NDOA KINYUME NA MAUMBILE.

•Hapa kuna watu ambao unaweza kukuta ni wanandoa ila wanafanya tendo la ndoa kinyume na maumbile, hii ni dhambi ya zinaa.

Lakini pia wapo ambao wanashiriki dhambi hii kama MASHOGA & WASAGAJI.

•Ushoga ni kitendo cha wanaume kukutana kimwili na usagaji ni kitendo cha wanawake kukutana kimwili. Ushoga na usagaji ni roho ambayo inaweza kumuingia mtu eidha kwa

kuangalia video chafu au kunuiziwa. Mungu amekataa watu wa jinsia moja kukutana kimwili.

***Mambo ya Walawi 18:22***

***[22]Usilale na mwanamume mfano wa kulala na mwanamke; ni machukizo.***

Suala la ushoga na usagaji limekuwa sasa ni la kidunia na ulimwengu wa giza umeweka mikakati ya kuhakikisha mataifa yanatoa hadi vibali na kuweka sheria ya kusimamia haki za watu hao, hii imepanuka mpaka kwenye baadhi ya makanisa ambayo yameanza kubariki ndoa za jinsia moja. Kwasasa upo umoja unaosimamia masuala ya jinsia moja (LGBT)

Haya ni machukizo makubwa sana na Nchi yeyote ambayo imehalalisha ushoga na usagaji imefananishwa na SODOMA na GOMORA ambao

waliangamizwa na Mungu kwasababu ya tabia hizo.

## 2.3 ZINAA NI MTU MMOJA KUAMUA KUJIRIDHISHA KIHISIA (KUJICHUA).

•Punyeto/kujichua ni kitendo cha mtu mmoja kujilidhisha hisia zake za kimwili, wapo wanaume ambao hutumia mafuta, sabuni au mikono yao kujichua pia wapo wanawake wanaotumia visanamu mbali mbali au vidole vyao kujiridhisha hisia zao, kiufupi ni kwamba hakuna mtu anayeweza kufanya Punyeto/kujichua kama ndani yake hana taswira ya mtu fulani ambaye anakutana naye kihisia. Watu wengi wameanza kujichua kwasababu ya video na picha chafu mtandaoni. Acha nikupe siri, hakuna mtu yeyote mwenye akili timamu ambaye anaweza kufanya

tendo la ndoa na akajirekodi na kuposti mtandaoni ili dunia nzima imuone, kwahio bila shaka huyu mtu anakuwa na roho za kishetani zinazomtawala na kumfanya kama ajenti wa kuzimu ili awavute wengi katika dhambi.

Kwahio kumbe mtu anayejichua kwa kutazama hizi video ukweli ni kwamba hazini na taswira za watu ila anakutana na majini mahaba uwanjani.

## 2.4 ZINAA NI UCHAFU WA KINGONO.

•Uchafu ni moja kati ya dhambi za zinaa, hii inaweza kuwa kutazama picha za uchi, video za ngono, kufanya sex-chat, kuongea matusi na story chafu, kusikiliza mazungumzo yanayochochea mapenzi, video call za uchafu na mengine kama hayo.  Uchafu huu unasababishwa na tamaa kali za mwili ambazo

mtu ameshindwa kuchukua hatua ya kuzidhibiti. Hizi tamaa ni roho chafu ambaazo zinakuwa ndani ya mtu.  Biblia inasema lakini uasherati usitajwe kwetu pamoja na uchafu wa kutamani ***(Waefeso 5:3)***

## 2.5 ZINAA NI ULAWITI & UBAKAJI.

•Ulawiti ni kitendo cha ubakaji kwa watoto lakini pia ubakaji unawezwa kufanywa hata kwa wakubwa, kwenye nchi za wenzetu hii aina ya zinaa ambayo mtu anakutana na vitoto vidogo wanaiita Pedosex. Matukio ya ulawiti/ubakaji yamekuwa yakisemwa katika vyombo vya habari na wafanyayo haya matukio hawafanyi tu kimwili bali haya yote huanzia rohoni (kwenye ulimwengu usioonekana).

Mtu yeyote anayepata mawazo ya KUZINI NA VITOTO vidogo huyo anatakiwa kusaidika na

NGUVU za MUNGU za kumsaidia zipo kwani biblia inasema wafiraji na walawiti wote hawataingia mbinguni ***(1 Wakorinto 6:9).***

## 2.6 ZINAA NI KUFANYA TENDO LA NDOA NA WANYAMA.

Kuna watu ambao wamefikia hatua ya kulala na wanyama, sio tu katika nchi za wazungu bali sasahivi hadi katika nchi zetu za kiafrika wapo ambao wanaishi na wanyama kama vile mbwa na wanawatumia wanyama hawa kukamilisha haja zao za kimwili.

# 3.0 NINI KINAMFANYA MTU AZINI.

Zinaa ni dhambi ambayo haianzi tu ‘automatically’ kuna visababishi vingi vinavyompelekea mtu hadi akazini. Nimekuanishia visababishi 10 hapa chini ambavyo vinawafanya watu waingie katika zinaa.

## 3.1 KUTAZAMA KWA KUTAMANI.

Kisababishi mama cha mtu kuingia katika zinaa ni tamaa ya mwili & macho, zinaa nzima imelala hapa. Mtu anapofaulu tu mtihani wa kuuweza mwili na tamaa zake basi hawezi kuzini kabisa.

Siku zote huwa nasema kuwa ni jambo moja kutazama lakini pia ni jambo lingine kutamani. Bwana Yesu alisema **kila amtazamaye**

**mwanamke akamtamani** amekwisha kuzini naye moyoni *(Mathayo 5:28)* Ni muhimu sana kuufundisha mwili wako na macho yako jinsi ya kuwatazama watu kama ndugu zako kwani wala sio shetani ila ni tamaa yako ndio huwa inakuvuta kwenye dhambi.

*Yakobo 1:13-14*

*[13]Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu.*

*[14]Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa.*

Uzinzi hauanzi kama kitendo, kitendo huwa ni kumalizia tu tukio ambalo tayari limeshaanza rasmi moyoni mwako kwa kutumia mawazo yako mwenyewe.

Bahati nzuri hili jambo halina jinsia, wote wanaweza kutamani.

### 3.1.1 Daudi alimtamani mke wa Uria.

*2 Samweli 11:2*

*[2]Ikawa wakati wa jioni, Daudi akaondoka kitandani, akatembea juu ya dari ya jumba la mfalme; na alipokuwa juu ya dari aliona mwanamke anaoga; naye huyo mwanamke alikuwa mzuri sana, wa kupendeza macho.*

### 3.1.2 Mke wa Potifa alimtani kijana Yusufu.

Hadi wanawake pia huwa wanatamani, mwanamke anaweza akamtamani mwanaume sio kwasababu tu ya uzuri au umbile bali

anaweza akatamani hata mafanikio ya huyo mkaka na hadi ikampelekea kuziwasha hisia zake za mapenzi juu ya kijana huyo kama ambavyo mke wa Potifa alivyomuona Yusufu Anastawi tu, kijana alikuwa anaonekana anakokwenda atakuwa bonge la tajiri.

*Mwanzo 39:7*

*[7]Ikawa baada ya mambo hayo, mke wa bwana wake akamtamani Yusufu, akamwambia, Lala nami.*

|Ikawa baada ya mambo hayo|

Je, ni mambo gani hayo?!  Ni mafanikio ya bwana mdogo Yusufu, kasome mistari iliyotangulia.

Nisikilize…

Mara nyingi uzinzi unaanzia machoni, unatazama nini? Kumbuka unachokitazama ndicho kinajaa ndani ya moyo wako, wapo watu ambao macho yao yamejaa uzinzi kiasi kwamba yeye anapotazama tu jicho linamuonyesha sex.

*2 Petro 2:14*

*[14]wenye macho YAJAAYO uzinzi, watu wasiokoma kutenda dhambi, wenye kuhadaa roho zisizo imara, wenye mioyo iliyozoezwa KUTAMANI, wana wa laana;*

Hii ndiomaana wanawake wameonywa wasiyachochee mapenzi kabla ya wakati

kwasababu miili yao imetengenezwa kwa namna fulani, wanatakiwa kustiri miili yao. (1Petro 3:3-6)

*Wimbo Ulio Bora 2:7*

*[7]Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu,*

*Kwa paa na kwa ayala wa porini,*

*Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha,*

*Hata yatakapoona vema yenyewe.*

**Usiamshe vilivyolala.**

AGIZO.

Jitahidi sana katika maombi yako usiache kabisa kuyaharibu mawazo mabaya kwani hizo ni ngome zinazotakiwa kuangushwa kabla ya mambo yote *(2Wakorinto 10:5).*

## 3. 2 MAZUNGUMZO MABAYA.

Mazungumzo mabaya ni moja kati ya visababishi vikubwa vya mtu kushikwa na zinaa, kuikimbia zinaa ni pamoja na kuyakimbia mazungumzo yote yanayoweza kukusababishia kuingia katika zinaa.

Chochote unachokisikia nyuma yake huwa kuna roho fulani, zinaa ni roho na watu wamempokea zinaa kupitia kile wanachokisikia nje.

Ni muhimu sana hata kuzingatia movie na nyimbo unazosikiliza kwani nyuma yake kunaweza kuwa na roho ya zinaa imekusubiri ikuingie.

*Ezekieli 2:2*

*[2]Naye aliposema nami, roho ikaniingia, ikanisimamisha; nikamsikia yeye aliyesema nami.*

Kuna watu ambao waliingia katika vifungo vya zinaa baada tu ya mazungumzo ya kingono, unakuta ni wachumba lakini wanapiga stori za mahaba, wengine utakuta usiku wa manane wanaongea kwenye simu, wanachati kingono na hadi wanapigiana video call.

Mazungumzo ya namna hii huwa ndiyo yanaharibu tabia ya mtu. Hata majina ambayo tunaitana, mtu hata mahali hujamyolea lakini unamuita My sweetheart,my honey. wewe unategemea usiamshe tu vilivyolala?

*1 Wakorintho 15:33*

*[33]Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema.*

Unaweza kukuta mtu ameokoka na bado anajiunga kwenye vikundi vinavyowajadili wanaume, unakuta wanawachambua wanaume, mwingine analeta mada za kutokuridhika kwenye tendo la ndoa na huyu anachangia la kwake, hapo lazima tu tabia zako zigeuzwe.

Maeneo ambayo utakuta mazungumzo mabaya ni kama vile BAR, GESTI, VITUO VYA KUBETI NA KAMARI na maeneo mengine kama hayo, ni bora kuyaepuka mapema. Usiende huko na wala kwenda kuomba ushauri kwao, ni bora muda mwingi ukae na neno la Mungu.

*Zaburi 1:1*

*[1]Heri mtu yule asiyekwenda*

*Katika shauri la wasio haki;*

*Wala hakusimama katika njia ya wakosaji;*

*Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.*

## 3.3 ROHO ZINAZOFUATILIA.

Matendo ya zinaa kama vile ndoa za wake wengi, kujichua, kuzaa kabla ya ndoa, kuchepuka, kutoa mimba, uasherati na mengine kama hayo yanaweza kabisa kusababishwa na roho fuatilizi kutoka kwenye ukoo.

Tabia huwa zinasafiri katika damu, ni rahisi kukuta mtu anafanana tabia na mzazi wake au ndugu zake kwasababu ya urithi wa damu kutoka

kizazi hata kizazi, haya sio tu mambo ya kiroho bali hata sayansi inatuambia hivyo kuwa huwa kuna mpitisho wa sifa fulani kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto (transfer of genetic traits from one genetation to the other)

NIKUPE MIFANO YA KWENYE BIBLIA.

3.3.1 Tabia ya Ibrahimu kuoa mke mzuri wa uso [beautiful] na kusema uongo kuwa yeye sio mmiriki haikuishia kwake tu, hii inshu ilifika hadi kwa watoto, Isaka naye alioa mke mzuri [Rebeka] na wakati anaulizwa kuhusu umiriki akasema yeye wala sio mumewe. *(Mwanzo 20:1-3; 26:7)*

3.3.2 Tabia ya uzinzi wa Yuda aliyelala na mkwe wake Tamari akidhani ni kahaba ilifika hadi kwa Daudi aliyelala na mke wa shujaa wake pia ndiyo ilifika mpaka kwa mwanaye Absolomu aliyelala

mpaka na wake za babaye lakini pia ilifika hadi kwa Amoni aliyelala na umbu lake Tamari *(Mwanzo 38, 2Samweli 11, 2Samweli 13)*

Kwahio basi mtu anaweza kabisa akajikuta ana tabia za zinaa ambazo zimetokana na ukoo wao na huyu mtu asipozishughulikia basi zitaendelea kutafuna kizazi hata kizazi.

Njia pekee ya kuweza kuondokana na hizo roho fuatilizi ni kwa kufunguliwa katika maombi na maombezi, unaweza kuwaona watumishi wa Mungu wenye neema hiyo na pia wewe mwenyewe binafsi ukaendelea kujikita katika mifungo na maombi ili kubadilisha hizo tabia.

Isaka ni mmoja kati ya watu wa kuigwa katika biblia kwani hakuridhika na hali ya utasa kwa mke wake Rebeka ambao ulikuwepo pia kwa mama

yake Sara aliyekuwaga tasa. Yeye Isaka hakuridhika kama baba yake bali aliingia kumuomba Mungu ili kubadilisha hio tabia.

*Mwanzo 25:21*

*[21]Isaka akamwomba BWANA kwa ajili ya mke wake, maana alikuwa tasa. Naye BWANA akamwitikia, na Rebeka mkewe akachukua mimba.*

## 3.4 WATU UNAOAMBATANA NAO.

Zinaa ni dhambi inayoambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda mwingine kwa wepesi sana, watu unaokaa nao wanaweza kukuamlia aina maisha ya kwamba uwe mzinifu au lah!

Kuna watu ambao walianza kuingia katika matendo kama vile kujichua, kutazama picha na video chafu na michezo mingine wanayoita kudeti kwasababu tu ya watu walioambatana nao.

Mimi binafsi ni ushuhuda kati ya watu walioharibiwa na watu nilioambatana nao enzi nasoma sekondari, hao ndio walionifanya namimi nianze kutazama picha chafu ambazo zilinigharimu muda mrefu kuja kuziacha.

Ogopa sana marafiki wanaokupelekea kuziwasha tamaa za mwili, kuna wengine ni contacts zako za whatsapp lakini post zao za STATUS hazina maadili, unakuta mtu anaangalia status za marafiki zake na akishatoka hapo tayari amewaka kihisia anaingia kujichua.

Naomba usome kisa hiki cha Amnoni na rafiki yake Yonadabu aliyemshauri kujiuguza ili alale na binamu yake kwani alimpenda.

*2 Samweli 13:3-5*

*[3]Lakini Amnoni alikuwa na rafiki, jina lake Yonadabu, mwana wa Shama, nduguye Daudi; naye Yonadabu alikuwa mtu mwerevu sana.*

*[4]Naye akamwambia, Kwa nini, Ee mwana wa mfalme, unakonda hivi siku kwa siku? Hutaki kuniambia? Amnoni akamwambia, Nampenda Tamari, umbu la ndugu yangu, Absalomu.*

*[5]Yonadabu akamwambia, Lala kitandani mwako ujifanye mgonjwa na babako atakapokuja kukutazama, umwambie, Mwache ndugu yangu, Tamari, aje, nakusihi, anipe mkate nile, akaandae chakula machoni pangu nikione, nikakile mkononi mwake.*

Mara nyingine mtu ni muhimu sana kujitenga, usipende sana kukaa kwenye makundi makundi ambayo ni rahisi sana kubadilisha tabia zako, haipendezi mtu aliyeokoka kujipeleka kwenye mabanda ya mpira, vijiwe vya kahawa n.k

*Mithali 13:20*

*[20]Enenda pamoja na wenye hekima, nawe utakuwa na hekima; Bali rafiki wa WAPUMBAVU ATAUMIA.*

## 3.5 KUISHI BILA MAONO/RATIBA.

Ni rahisi sana mtu kuingia katika dhambi hasa za zinaa kama anaishi kiholela tu bila ratiba yeyote. Kila siku uliyonayo ni rasilimali kubwa sana ambao Mungu amekupa kama mtaji wa kuanzia.

Kuna watu ambao wao huwa wanaongelea mambo ya mwakani nitafanya hiki na kile, baada ya miaka mitatu nitafanya hiki na hiki na mtu anashindwa kuelewa kwamba maisha anayoyataka baada ya mwaka mmoja ni zao la siku moja moja 365 anazozithamini na kuzifanyia kazi kwa bidii na kwa mpangilio.

Maskini wote na wenye dhambi hasa zinaa ni watu ambao hawathamini muda wao, mtu yuko tayari kwenda kunyoosha miguu au kupoteza-poteza muda kuliko kujitenga na kuutumia muda

wake vizuri katika kujiongezea maarifa na kufanya kazi zake kwa bidii.

Baba yangu wa kiroho Bish Dickson Cornel Kabigumila aliwahi kusema leo ni siku sahihi ambayo ungevuna miti uliyopanda miaka 20 iliyopita lakini pia leo ni siku sahihi ambayo ukipanda miti utaivuna miaka 20 ijayo.

Chanzo cha uzinzi wa Daudi ilikuwa ni kukaa tu bila ratiba yeyote, akaamua kuichezea siku moja, wakati ambapo wafalme walikuwa wanatoka kwenda vitani yeye akabaki tu nyumbani anapoteza-poteza muda na baada ya hapo ndipo alipoanguka katika zinaa.

*2 Samweli 11:1-2*

*[1]Hata ikawa, mwanzo wa mwaka mpya, wakati watokapo wafalme kwenda vitani, Daudi akampeleka Yoabu, na watumishi wake pamoja*

*naye, na Israeli wote; wakawaangamiza wana wa Amoni, wakauhusuru Raba. Lakini Daudi mwenyewe akakaa Yerusalemu.*

*[2]Ikawa wakati wa jioni, Daudi akaondoka kitandani, akatembea juu ya dari ya jumba la mfalme; na alipokuwa juu ya dari aliona mwanamke anaoga; naye huyo mwanamke alikuwa mzuri sana, wa kupendeza macho.*

RATIBA ZA KUWEKA NDANI YA SIKU.

I)KUOMBA (walau kwa nusu saa asubuhi mchana na usiku)

II)KUSOMA NENO (Walau aya tatu kila siku)

III)KUSIKILIZA MAFUNDISHO (Walau audio/video 3 kila siku)

IV)MIFUNGO (Walau siku 3 kwa wiki)

V)KUSOMA VITABU (Walau kimoja kila mwezi)

VI)FANYA KAZI KWA BIDII (Kazi ni kuweka katika matendo kila wazo la Mungu ndani yako)

Ukiyafanya hayo sio tu utaikimbia zinaa bali  pia ndio kanuni zinazowafanya watu wafanikiwe katika haya maisha.

Zinaa utaishinda kwa kuwa bize, ishi na maono kwani usipokuwa na maono UTAFANYA KILA KITU.

*Mithali 29:18*

*[18]Pasipo maono, watu huacha kujizuia;*

*Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.*

## 3.6 MAHUSIANO KABLA YA WAKATI.

Kuna watu ambao wameingia katika mambo ya uasherati kwasababu tu ya kuingia katika mahusiano wakati usiokuwa sahihi, unakuta mtu hajui hata anahitaji kufunga ndoa lini ila eti yupo kwenye mahusiano [wanaita Dating].

Mahusiano ya uchumba yeyote yasiyokuwa na maono yanayoeleweka kuelekea kwenye ndoa ni moja kati ya nyenzo nzuri sana ambazo shetani anazitumia kuwavuta vijana wengi katika dimbwi la zinaa!

Kukaa kwenye uchumba miaka mingi halafu utegemee kuikimbia zinaa ni majaribu ambayo siku moja yatakuzidia, cha ajabu sasa ndani ya uchumba huo utakuta mnaanza hadi kufundishana jinsi mtakavyokuwa mnafanya

tendo la ndoa, mwingine anaangalia hadi video chafu ili tu abaini njia za kumtetea mwenzake katika mahaba [Hahahahahahaa]. Hiyo sio ndoa tena ni ndoano ambao shetani anajivunia miaka michache baadaye.

Kipindi cha uchumba ni kipindi hatari sana, katika kipindi hiki ni muhimu sana sana mtu kuzingatia kanuni zinazotawala uchumba kwa kujisomea vitabu muafaka. Mahusiano yoyote ya kisirisiri hayatakiwi. Wekeni wazi uhusiano wenu kwa wazazi wa kiroho na kimwili.

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UCHUMBA ILI KUJILINDA NA ZINAA.

i)Hakikisha unatenga muda wewe na mwenzako na huo muda mnautumia kuomba na kujadili

neno, hata kama ni kwenye simu jitengeeni walau nusu saa kila siku.

ii)Hakikisha unakuwa na ratiba inayoeleweka na sio kila saa mnachati tu, kila saa mnaongeaongea kwenye simu, hii huwa ni hatari sana.

iii)Hakikisha mnakuwa na ratiba ya kusoma vitabu au kusikiliza mafundisho pamoja na mwenzako, mnapangiana kabisa kwamba wiki hii au mwezi huu tutasoma hiki na baada ya hapo mnafanya hitimisho pamoja na kuyaweka hayo katika matendo.

iv)Hakikisha mnajiripoti kwa wazazi wa kimwili na kiroho na watu muhimu baadhi ili mkae katika ulinzi, mahusiano yeyote yasiyokuwa na walezi ni hatari sana na ni rahisi kuanguka katika dhambi.

v)Hakikisha mnakuwa na maono yanayoeleweka katika maisha yenu ya baadaye, mtafanya nini baada ya miaka fulani na yote yanayohitajika kwaajili ya maisha ya baadaye.

## 3.7 MATUMIZI MABAYA YA TEKNOLOJIA

Zinaa ni dhambi pekee inayokuwa kwa kasi duniani kuliko dhambi nyingine yeyote. Kipindi Bwana Yesu alipokuwepo duniani kimwili aliwahi kukiri kwa kinywa chake kuwa kile kizazi kilikuwa ni kizazi cha uzinzi na dhambi *(Marko 8:38),* Yaani hakudiriki kuijumuisha zinaa katika dhambi zingine na badala yake akaipa upekee wake kwasababu yamkini aliyokuwa anayaona yanaendelea kwa wakati huo katika hii sekta ya zinaa yalimshangaza mno.

Sasa ikiwa Bwana Yesu alikiri mwenyewe kuwa kile kizazi kilikuwa ni cha uzinzi na dhambi Je, vipi kuhusu sasa?! Wote tunafahamu kuwa nyakati hizo hakukuwa hata na smartphone, hakukuwa na internet kama wakati huu ambapo zinaa mtu anaweza kuikamilisha chumbani kwake tu kwa kujiangalizia video na picha chafu.

Sayansi na teknolojia vimetuletea zinaa karibu yetu zaidi [zinaa kiganjani mwako]. Kwasasa kijana mdogo tu tena wa shule ya msingi anamiriki simu yenye internet na anaperuzi kila kitu. Watoto wadogo wanakalishwa kwenye katuni ambazo wakati mwingine utakuta zinaa inatangazwa wazi wazi, kwahio mtoto mdogo anajua kukumbatia, anafahamu kuhusu kiss na jinsi inavyofanywa, na cha ajabu haya yote anayoyaona hapati watu wazima wa kum-coach.

Sayansi na teknolojia sio kitu kibaya ila tusipojua matumizi mazuri ya huu utandawazi basi kizazi chetu kitakuwa hatarini sana katika dhambi hizi za zinaa kwani mtandaoni kwasasa kuna hadi madalali wa ngono, kuna makungwi wanaofundisha stayle za mapenzi na mambo kama hayo, kuna application za kutaftia wapenzi (madanga), kila kitu ni zinaa tu, kwenye bongo fleva ni uzinzi, kwenye movie ndio usiseme na hata katika mabango  ya matangazo unakuta mtu yupo uchi.

MAMBO YA KUCHUKUA TAHADHARI.

i)Endapo una akaunti yako FACEBOOK, INSTAGRAM, YOUTUBE, TIK-TOK na sehemu zingine hakikisha unaingia kutafuta taarifa zitakazokuongezea thamani, usimtazame kila mtu, hakikisha una watu fulani unaowafuatilia,

ukikutana na picha au video chafu Scrol fasta, usitulie kabisa kuangalia, pita kama vile huoni. [Pita kama mshale]

ii)Endapo una application ya WHATSAPP usiwe na magrup yasiyokuwa na maadili, punguza idadi ya magrup, mwingine unakuta ana grup hadi la aliosoma nao shule ya msingi na mambo yanayojadiliwa humo ni upuuzi tu. Pia hakikisha hauvutwi kwenye uraibu wa kuangalia STATUS hovyo, huko status ni rahisi kukuta mahudhui ya hovyo na yakakubadilisha mtazamo wako ndani ya muda mchache sana.

iii)Tambua namna nzuri ya kutumiana ujumbe mfupi [CHATING], mfumo huu umepanuka sana, kwasasa kwenye mitandao wamekuongezea kitu kinaitwa IMOJI, usitumie hovyo hizi imoji kwani kuna watu wamewasha tamaa zao kwasababu tu

ya imoji na STICKERS. Kuna vile viimoji vya kuziba macho kuonyesha aibu, kuna zile za lips n.k. Ukiwa Mesenja,Telegramu, Whatsapp n.k jitahidi sana uwe na kiasi katika kuchati, usichati na kila mtu na usipoteze zaidi ya dakika tano upo unachati na mtu, kuna mtu unakuta hata mambo anayochati ni ya kijinga tu mfano UMEKULA NINI? UMEVAAJE? VIPI UMELALA STYLE IPI? [Haya mazungumzo ni hatari sana na ndio yanawapelekea watu kuanguka katika zinaa]

iv)Hakikisha hautumii VIDEO CALL kiholela, watu wengi wameanguka katika zinaa kwasababu ya hizi video call, mtu alianza mazungumzo vizuri lakini kadri muda unavyoenda anaanza kushawishika kukuona mwili wako, kuona miguu mara mapaja. Kamwe usiendekeze haka ka mchezo ni hatari kwa afya yako.

v)Pangilia muda wako wa kufanya mazungumzo na mtu hata kama ni kwanjia ya NORMAL CALL, hasa kwa wale ambao hawajaingia katika ndoa wanatakiwa kuratibu muda wa kuwasiliana vizuri, huu mtindo wa kupigiana simu tena usiku mnaongea masaa yanakata tu, mwingine hadi anachomeka simu kwenye chaji, simu inachemka ila yupo tu.  Hii ni hatari sana.

## 3.8 KAZI/BIASHARA [MAENEO] HATARISHI.

Kuna aina fulani za kazi/biashara ambazo mtu akifanya anakuwa kwenye hatari kubwa ya kuvamiwa na matendo ya zinaa.

Kuna mtu mwingine anashindwa kabisa kuondoka kwenye zinaa kwasababu ya aina ya kazi alizozichagua au kukaa katika maeneo hayo.

MFANO WA KAZI/MAENEO HAYO:

i) Meneo ya walevi [Bar] na Disco.

Haya ni maeneo hatari sio tu kwa kufanya biashara hii bali hata kuwa tu kwenye mazingira haya kunaweza kumsababisha mtu akaanza kuingia kwenye uasherati. Bar/disco sio eneo la starehe wala sio eneo la kupumzikia na kula raha

kwasababu mtu anaenda akiwa mzima anatoka na roho chafu za zinaa na nyinginezo.

ii)Nyumba za kulalia wageni [Guest house]

-Moja kati ya maeneo hatarishi sana kwenye kueneza zinaa ni hizi nyumba za kulalia wageni, hizi nyumba hazina ubaya wowote kama zikitumiwa katika wema ila kwa dunia yetu ya sasa asilimia kubwa ya matumizi ya nyumba hizi huwa ni katika zinaa. Kwahio ni muhimu sana kwa mtu ajilinde na haya maeneo hasa hasa wale wanaotamani kufanya kazi kama wahudumu wa guest house [iweni na tahadhari hii]

iii)Maeneo ya beach.

-Kuna watu ambao tangu siku ile alipoenda beach aliondoka na roho za zinaa. Kwenda kwenye maeneo ya beach/ufukweni sio dhambi na wala si vibaya ila kwawewe usiye na nguvu rohoni ujiandae kumezwa na roho chafu zilizoko huko kwani shetani amewekeza kwa kiasi kikubwa katika maeneo hayo. Haya sio maeneo ya starehe ila ni maeneo ya karaha kwani huwa yanasababisha sana mabaya.

iv)Kazi za ndani [House boy & Girl]

-Nimeshuhudia na kupokea kesi nyingi sana za uzinzi kutoka kwa hawa dada  wa kazi. Wengi wao huwa wanashawishiwa sana katika dhambi ya zinaa, ni wachache sana walio salama. Hata wanaume pia [shamba boy] huwa wanakutana na kitu hiki, Yusufu ni mfano mzuri wa mtu aliyekuwa mtumwa katika nyumba ya Potifa na

akatamaniwa katika zinaa na mke wa mzee wa nyumba *(Mwanzo 39:1-10)*

v)Udereva wa masafa marefu [Maeneo ya parking]

-Pasipokuwa na uimara wa mtu rohoni ni rahisi sana kukuta madereva wengi hasa wa haya magari makubwa kutumiwa na adui katika eneo la zinaa, wengi wao huwa ni wazinzi na adui huwatumia wengi wao kama mawakala wa kusambaza roho za zinaa na magonjwa ya zinaa. Ukikuta eneo ambalo haya magari yanapaki huwa kuna roho za zinaa kwa kasi sana.

NYONGEZA.

-Pia zipo kazi na biashara zingine ambazo wanaozifanya inabidi wawe na tahadhari kubwa mno kwani ni rahisi wao kunaswa katika zinaa

mfano Ualimu, udaktari, unesi, ukatibu/uhasibu hasa kwenye ofisi za maboss na mwisho ni maeneo ya makahaba ambayo tunatakiwa kuyaepuka.

## 3.9 MAJIRA NA NYAKATI HATARISHI.

Moja kati ya visababishi vya zinaa ni majira na nyakati hatarishi. Kuna majira na nyakati ambazo itakubidi uwe makini kwani wapo watu walioingia kwenye zinaa kwa kupuuzia majira hayo.

Kwamfano nyakati za JIONI/USIKU.

Dhambi nyingi hasa zinaa huwa zinafanyika wakati wa usiku. Zinaa inafanyika sana wakati huo kwasababu ni jambo la siri, mtu anayezini huwa anajificha ili asionekane na watu.

Ukiachana na Daudi ambaye naye alishawishika kwenye zinaa nyakati za jioni lakini pia kuna kijana maandiko yanasema ni mjinga ambaye alikutana na kahaba nyakati za usiku na akanaswa katika uzinzi kirahisi sana.

*Mithali 7:7-10,21-22*

*[7]Nikaona katikati ya wajinga,*

*Nikamtambua miongoni mwa vijana,*

*Kijana mmoja asiyekuwa na akili,*

*[8]Akipita njiani karibu na pembe yake,*

*Akiishika njia iendayo nyumbani kwake,*

*[9]Wakati wa magharibi, wakati wa jioni,*

*USIKU WA MANANE, GIZANI.*

*[10]Na tazama, mwanamke akamkuta,*

*Ana mavazi ya kikahaba, mwerevu wa moyo;*

*[21]Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi,*

*Kwa ubembelezi wa midomo yake akamshinda.*

*[22]Huyo akafuatana naye mara hiyo,*

*Kama vile ng'ombe aendavyo machinjoni;*

*Au mpumbavu kuadhibiwa katika pingu;*

Ni vizuri kujiepusha katika matembezi ya kiholela hasa hizi nyakati za usiku, usiku huwa unapumbaza sana akili za watu, ni rahisi mtu kujisahau na akajiona kana kwamba hakuna anayemuona ilihali Mungu anaona mpaka gizani. Kuna majira mengine kama majira ya baridi, majira ya furaha kubwa [Great excitement] mtu anatakiwa kuwa na tahadhari ya zinaa.

Nimewahi kumsikia mtu aliyekuwa ameokoka na akaingia  katika zinaa kwa mara ya kwanza kabisa

kwasababu tu ya kupewa zawadi ya maua na mchumba wake, hiyo siku alizidiwa kwa furaha, yalikuwa ni majira hatari kwake.

Majira mengine ni siku za sikukuu kwamfanao siku ya VALENTINE, hii ni siku ambayo huwa inaenda na baadhi ya watu na wala sio vijana tu, utakuta hata watu wazima hii ndio siku yao ya kufanya maovu, siku ya kuiga kinachofanywa duniani. Kuna wengine wamejikuta ni wanandoa lakini majira na nyakati zimewafanya wafanye tendo kinyume na maumbile [Huu ni uovu mkubwa]

Lakini pia kuna majira ya kibiolojia japo sio kwa umuhimu sana, kumekuwa na watu wanaoingia kwenye zinaa vipindi vya balehe wengine wanawake watakwambia wakiwa katika siku zao

wanapata hisia kali.  Hii inatibiwa na maisha ya maombi na mifungo, huwezi kushinda kujizuia.

Pia kuna siku za harusi na sherehe zingine nyingi ambazo huwa zinawapumbaza watu na hata wakajikuta wamenaswa na zinaa, weka tahadhari kubwa ndugu yangu unaweza ukapoteza maisha yako ndani ya siku moja tu.

## 3.10 KUTAFUTA UNAFUU WA MAISHA.

Kama unatambua kuwa tupo katika kizazi cha zinaa na ya kwamba zinaa imeshika kasi kila eneo katika maisha basi ni muhimu kwako kujipanga dhidi ya maisha, ujue namna utakavyotimiza mambo yako bila kuwa tegemezi kwa wanye navyo.

Sikuhizi za mwisho shetani anainua watu wengi wenye pesa na mamlaka katika nyanja tofauti tofauti ili akunase wewe mwenye hali ngumu ambaye utatamani mafanikio hata kwa kuingia katika zinaa.

Kuna watu wengi na hata watumishi wa Mungu pia ambao wameingia katika maagano ya zinaa kwasababu ya kupewa nguvu na umaarufu katika maeneo yao ya kihuduma.

Nilikuwa namsikiliza Baba yangu Askofu Dickson Cornel Kabigumila anasema kuwa katika kizazi hiki unaweza kukuta mtumishi wa Mungu analala na hao wanae wa kiroho wanaomuita Baba baba, kumbe hata hakuna cha baba ni wake zake kabisa na wanafanya zinaa.

Lakini pia kuna kundi kubwa hasa wanawake ambao huwa wanashawishika kuingia katika zinaa kwasababu ya kuahidiwa pesa au kwasababu ya kuona mali za mwanaume, kuna mwingine ili apewe kazi fulani utamkuta anakubali kutoa hongo ya mwili wake.

Hata makahaba wapo ambao waliingia katika biashara hizo kwasababu ya hali za kiuchumi, wanawake wengine wameingia katika ndoa za wake wengi kwasababu ya kutafuta unafuu wa kimaisha. Njia za uzazi wa mpango mfano matumizi ya kondomu n.k ni moja kati ya visababishi vya zinaa, kuna watu wameingia katika zinaa kwasababu ya kuwepo tu kwa hivi vitu, vimewafanya warahisishe maisha.

Naomba nikushauri kitu huwezi kufanikiwa kwa kutegemea pesa zinazopatikana kwasababu ya zinaa (Kutoa mwili wako).

Mafanikio ya namna hii ya kuwategemea "malaya" huwa hayadumu, maisha yatakupiga mpaka utafikia hatua ya kukoswa mpaka pesa ya chakula [kipande cha mkate]

*Mithali 6:26*

*[26]Maana kwa malaya mtu hutiwa katika hali ya kuhitaji kipande cha mkate;*

*Na kahaba humwinda mtu anase nafsi yake iliyo ya thamani*

Nimewahi kusikia mdada mmoja anasema kuwa wakati anaishi maisha ya zinaa alikuwa na pesa nyingi sana kutoka kwa mwanaume [Danga lake]. Sasa kipindi ameamua kuishi maisha mazuri hajui hata hizo mali ziliteketeaje, shetani huwa

anachukua kila cha kwake halafu unaanza mwanzo.

# 4.0 HATUA UTAKAZOPITIA KABLA YA KUZINI.

Uzinzi sio tukio la bahati mbaya, kabla ya kuzini kuna ishara zitakazokuonyesha kuwa unaelekea kuzini!

Kabla DAUDI hajaingia katika zinaa na Bath-sheba mke wa Uria kuna hatua kadhaa alizozipitia *[2 Samweli 11:1-4]*

## 4.1 KUTAZAMA/KUSIKIA.

Watu wote walioingia katika zinaa walianza kwa kuona au kusikia, maana yake kama mtu hana macho na masikio hawezi kushawishika na zinaa!

Kila mtu/kitu ambacho utakiona/kukusikia na kikakuvuta katika zinaa ni adui namba moja anayekufanya uzini.

Kwa upande wa Daudi yeye alitazama uchi wa mwanamke akioga lakini hakuishia hapo bali maandiko yanasema yule mwanamke alikuwa mzuri sana na wa kupendeza macho. Hata kwa mke wa Potifa ndivyo ilivyokuwa, Yusufu alikuwa mzuri wa uso *(Mwanzo 39:6-7)*

## 4.2 KUTAMANI.

Hatua ya pili kuelekea uzinzi baada ya kutazama/kusikia ni kutamani, ni jambo moja kutazama na ni jambo lingine kutamani. Watu wote waliozini kwa vitendo walianza kwanza kuzini moyoni kutokana na picha walizoziona au sauti walizosikia, hiki ndicho alikisema Bwana

Yesu katika *(Mathayo 5:27-28)* ukimtazama mwanamke kwa kumtamani umekwisha kuzini naye moyoni.

Baada ya Daudi kumtazama mke wa Uria alimtamani na kama angeishinda tamaa wala asingezini kabisa, kumbe uzinzi sio bahati mbaya, uzinzi unaanza pale mtu anapoanza kutengeneza mawazo mabaya ambayo kwa mujibu wa 2 Kor 10:5 yanaweza kuangushwa na kuteketezwa katika maombi.

## 4.3 MAONGEZI.

Baada ya kumtamani mtu katika zinaa hatua inayofuata ni maongezi, mtu anapokuwa katika hii hatua ya tatu ataanza kuwasiliana na mtu kutokana na msukumo wa hisia za zinaa zilizoko ndani yake, hapa utakuta watu wanapigiana simu

usiku, wanachat mambo yasiyo na maana, wanaitana majina ya mahaba n.k

## 4.4 MIGUSANO/KISSING.

Nimeiweka hii kuwa miongoni mwa hatua za zinaa kwasababu wapo watu ambao wanasema kuwa hawazini ila wanafanya tu romance [Kupapasana, kubusiana]. Mtume Paulo anasema kwa habari ya mambo ya zinaa ni heri mwanaume asimguse mwanamke *(1Kor 7:1)*

Katika kizazi hiki hatua hii inaweza pia kuwa vitendo vya kutumiana picha za utupu na kupigiana video call za kingono zinazowapelekea kujichua/masterbation. Ukiona umefikia hii hatua tambua kuwa ni muda mfupi tu mtakutana na kuzini.

## 4.5 KUPANGA ENEO LA KUKUTANIA

Hii hatua ya mwishoni kabisa kabla ya kuhitimisha zoezi la zinaa. Watu wanaojikuta wameanguka katika zinaa huwa walianza kutengeneza mazingira hatalishi kwa wao kukutana au kukaa.

Kuna maeneo na nyakati  ambazo ni hatarishi mfano kukutana nyakati za JIONI au USIKU, hata Daudi naye ilikuwa ni wakati wa jioni aliposhawishika.  Mahali pengine wamemtaja kijana mmoja mjinga ambaye alikutwa na mwanamke aliyevaa mavazi ya kikahaba na huo ulikuwa wakati wa usiku *(Mithali 7:7-10)*

## 4.6 KITENDO CHENYEWE.

Mwisho wa mambo yote sasa mtu ndio huwa anadiriki kukamilisha kitendo cha kuzini na mtu, hili tendo wala halichukui muda mrefu ila mtu anapokutana hata kwa hizo dakika chache basi majuto huwa yanakaa kwa muda mrefu. Zinaa sio dhambi ya kawaida, Zinaa ndio dhambi pekee ambayo maandiko yanasema inatendwa juu ya mwili wa mtu *(1Kor 6:18)* zinaa huwa inamuondoa Roho Mtakatifu ndani ya mwili wa mtu ambao ni hekalu la Roho Mtakatifu *1Kor 6:19.*

# 5.0 ZINAA INAMFANYANINI MTU.

## 5.1.ZINAA INAHARIBU MWILI.

Mwili wa mtu ni wa thamani sana na zinaa ni dhambi inayoweza kusababisha uharibifu mkubwa sana katika mwili wa mtu

*1 Wakorintho 6:18*

*[18]Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi JUU YA MWILI wake mwenyewe.*

Je, zinaa inaharibuje mwili?

•Ni rahisi kupata mimba zisizotarajiwa ambazo zinaweza kuleta changamoto/complication kwa mwanamke. Wanawake wengi pia wanasumbuka sana changamoto za uzazi eidha kwa matumizi ya uzazi wa mpango mfano; P2 na SINDANO ZA MAJIRA.

•Ni rahisi kupata magonjwa ya zinaa mfano Ukimwi, UTI sugu, PID, Fangasi, kaswende, Uvimbe kwenye kizazi n.k

•Roho Mtakatifu huwa anaondoka kutoka kwenye mwili wa mtu anayezini.

Mwili wa mtu ni hekalu la Roho Mtakatifu

*(1Kor 6:19)*

Na kwasababu Roho Mtakatifu huwa anajihusisha kwenye KUHUISHA mwili *(Rum 8:11)* basi mwili wako utakuwa katika hali za

magonjwa na umauti. [Hautakuwa na msaada wa Roho Mtakatifu]

## 5.2 ZINAA INAHARIBU NAFSI.

*Mithali 6:32*

*[32]Mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa;*

*Afanya jambo litakalomwangamiza nafsi yake.*

Nafsi ya mtu huwa ina sehemu tatu ambazo ni:-

### 5.2.1 AKILI

Akili/mind ni sehemu ya muhimu sana katika nafsi ya mwanadamu, hapo ndipo Mungu huwa anawekeza uwezo mkubwa sana

unaomtofautisha kati ya mtu na mtu, hapo ndipo ambapo mtu atatakiwa apajaze MAARIFA sahihi ili kuzalisha vitu vikuu vilivyowekwa ndani yake.

Mtu apoanza uzinzi tu maandiko yanasema kuwa anakuwa HANA AKILI KABISA, kwahio kumbe zinaa inamfanya mtu aishi maisha chini ya viwango, unakuta mtu anafanya mambo ambayo hata hakutakiwa kuyafanya kwasababu ya zinaa.

Mfano mzuri ni kijana kwenye kitabu cha *Mithali 31:6-26* aliyegeuzwa njia zake na mwanamke aliyezini naye. Mwingine ni Sulemani na Samsoni waliogeuzwa mioyo yao na wanawake.

Huku kutokuwa na akili ndiko kunaweza hata kumsababisha mwanamke anayezini aanze mpaka kumpa kijana pesa nyingi, mwingine hadi

anamfungulia biashara mwanaume, huku ndiko KUHARIBIKIWA NA AKILI tunakokumaanisha.

### 5.2.2 HISIA.

Hisia ni muhimu sana kwa mwanadamu hasa linapokuja suala la mahusiano ya ndoa, huwezi ukaifurahia ndoa yako kama huna hisia na mwenzako, watu wengi wanajiingiza kwenye masuala ya zinaa tayari wanafanya jambo linaloangamiza hisia zao.

Mtu ambaye anatembea na wengine katika tendo la ndoa anapokuja kwa mwenza wake anaanza kumuona HANA RADHA, anaanza kumlinganisha na fulani kwasababu ya zinaa.

Kuna wanawake wengi ambao unakuta unanitafuta ananiambia dokta nisaidie mimi sina hisia kabisa na wanaume, anashindwa kuelewa kuwa tangu siku zinaa ilipoingia kwenye ndoa yake tayari hisia zake ziliharibiwa na adui.
*(Yohana 10:10)*

### 5.2.3 UTASHI.

Utashi ni uwezo wa mtu kufanya maamuzi au kuchukua hatua katika maisha.  Watu wengi wameharibikiwa na utashi wao kwasababu ya zinaa, unakuta mtu anajichua, anaangalia picha za uchi, video za uchi, anapigiana simu za uchafu na mchumba wake. Huyu hawezi kuwa na uwezo wa kufanya maamzi sahihi katika maisha.

Mwili wa mtu ni hekalu la Roho Mtakatifu na maandiko yanasema yeye anayezini huwa

anauharibu mwili ambao ni makao ya Roho Mtakatifu *(1Kor 6:19)* ambaye ndiye huwa anatusaidia kufanya maamzi sahihi.  Kwahio basi mtu yeyote aliyeamua kuingia katika zinaa anamuondoa Roho ndani yake na kubaki anafanya maamzi yasiyokuwa na usahihi.

Unashindwa kuacha zinaa nitafute nitakusaidia.

## 5.3 ZINAA INAHARIBU ROHO YA MTU.

Tumejifunza mwanzo kuwa zinaa ndio dhambi pekee ambayo huwa inahusisha sehemu zote tatu za mtu, NAFSI, MWILI na ROHO na ndiomaana hii dhambi inapofanyika huwa mtu hawezi akawa na mawazo au mazungumzo

mengine tofauti na kinachofanyika, hili jambo ni IBADA KAMILI ya kishetani kama likifanyika nje ya ndoa au kwa isivyostahili.

Mwanzo tumeangalia madhara ya zinaa katika mwili tukaangalia katika nafsi na leo naomba nikupe madhara ya kiroho, Zinaa ina madhara makubwa kiroho kwasababu yeye afanyaye zinaa mwisho wa roho yake ni jehanamimu ya moto.

*Waebrania 13:4*

*[4]Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.*

Kuna mtu mwingine yupo katika zinaa na anachoendelea kujifariji hadi asiache ni kuona yamkini bado ana miaka mingi mbele ataacha na atatubu.

Acha nikupe siri, siku zote dhambi ya zinaa huwa sio ya kuacha kirahisi na ndiomaana watu wanaosumbuliwa na KUJICHUA, KUTAZAMA PICHA CHAFU n.k ukiwauliza watakupa majibu kamili kuwa zinaa nibrahisi sana kuianza ila kuiacha ni mpaka neema ya kipekee, ni ngumu sana kuacha zinaa kwahiyo unaweza ukajikuta tayaru umeshaingia Jehanamu kirahisi sana.

## 5.4 KUPUNGUKIWA NGUVU ZA ROHONI

Moja kati ya hasara kubwa za zinaa ni mtu kugawa nguvu za rohoni alizojikusanyia ndani ya Mungu ambazo ndizo zinampa uimara wa kustahimili kila vita vya adui na mafanikio ya kila namna.

Hii ndiomaana Mfalme Lemueli anaambiwa na mama yake kuwa asiwape wanawake nguvu zake.

*Mithali 31:3*

*[3]Usiwape wanawake NGUVU zako;*

*Wala moyo wako usiwape wale wawaharibuo wafalme.*

Kumbe zinaa ni jambo linaloweza kumfanya mtu akampoteza Mungu na nguvu zake. Hii ni

teknolojia ambayo anaitumia sana shetani, akiona mtu anafanikiwa katika uchumi au mambo ya kiroho anatafuta kumletea kabinti ili azini au kamkaka ili ajimalize mwenyewe

Yusufu wa agano la kale yaliwahi kumkuta pia, baada ya kuwa ameuzwa kwa Potifa na ya kwanza maisha yake yameanza kustawi basi mke wa bwana wake aliingiliwa na shetani ili akimtamani tu Yusufu na kulala naye basi anakuwa ndio kampoteza Mungu wake.

*(Mwanzo 39:1-7)*

Haya ndiyo yaliyomkuta hadi Samsoni aliyetobolewa macho, aliwapa wanawake nguvu zake na habari yake ikaishia hapo *(Waamuzi 16)*

Hiki ndicho huwa kinatokea hata kwenye NDOTO ZA MAPENZI. Teknolojia huwa ni ile ile ya

kuwapunguzia watu nguvu za Mungu, kwahio ukiona umezinishwa ndotoni tambua kuna kiwango fulani cha nguvu za Mungu kinaondoka.

## 5.5 INAMUONDOLEA MTU HESHIMA YAKE.

Heshima ni hali inayomfanya mtu kudhihilisha uthamani wake katika dunia yake, mtu anapoheshimika inamaana hata mambo yake yote yatathaminika. Heshima ikiondoka kwa mtu anabaki anadhalaurika mtaani.

Zinaa ni dhambi inayoondoa heshima ya mtu, pale mtu anapoanza kuzini tu anaanza kupoteza thamani yake katika jamii, hakuna sifa nzuri kwa mzinzi.

*Mithali 6:32a-33*

*[32]Mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa;*

*[33]Atapata jeraha na kuvunjiwa heshima;*

*Wala fedheha yake haitafutika.*

## KISA CHA UZINZI WA AMNONI NA TAMARI NA AIBU YAO.

Nimesema zinaa ni tendo linaloweza kumvunjia mtu heshima kabisa na hasa hasa mtu ambaye NI MWAMINI, huwa ni hatari sana kwasababu unaweza ukawa umefichaficha ila hakuna jambo ambalo litafichika milele, utajulikana tu ndiomaana hata Daudi alipotaka kufuta ushahidi kwa kumuua Uria baada ya kuzini na mke wake wala haikufichika. Kuna watumishi wa Mungu

ambao wamepoteza heshima zao baada ya kesi za uzinzi.

Niwape tahadhari nyie vijana ambao MNATEMBELEANA MAGETONI.

Tamari pia alikuwa ni binti ambaye alidiriki kwenda getoni kwa Amnoni binamu yake ili eti akampikie chakula wakati alipokuwa mgonjwa, nakwambia kilichompata kasome *2Samweli 13:1-22,* Walizini na heshima yao ikaondoka.

## 5.6 ZINAA HUSABABISHA MAUAJI.

Mauaji yanayoweza kutokea baada ya zinaa ni KUTOA MIMBA, KUJIUA na KUUA.

Kuna mabinti wengi ambao wamekuwa wahanga wa kutoa mimba kwasababu ya zinaa mpaka wamesahau kama kutoa mimba ni dhambi ya

kuua. Wengi sasahivi wasipoangukia katika janga la utoaji mimba utakuta wanatumia uzazi wa mpango kama vile kuweka vijiti, vitanzi, kutumia kondomu n.k wasijue kwamba huu ni mpango wa shetani kuharibu vizazi vyao.

Lakini pia ukisoma katika maandiko utakutana na habari ya uzinzi wa Daudi ambao ulipelekea mauaji ya Uria. Wapo watu ambao huwa wanaingia gharama za kufanya mabaya kwa watu kwasababu ya zinaa na hofu ya zinaa. *(2 Samweli 11:1-13)*

Lakini pia kumekuwa na wimbi la watu kujinyonga au kunywa sumu kwasababu ya mapenzi na ukifuatilia utakuta taarifa za kwamba mtu ametoka nje ya ndoa na kumdanganya mwenzake.

## 5.7 ZINAA INAHARIBU HATIMA YA MTU.

Zinaa ni teknolojia ambayo shetani anaitumia sana kuharibu future ya mtu, nibrahisi kukuta mtu tayari amejipata na ameanza kutumika katika eneo sahihi ila shida inakuja pale tu anapoanza kuzini, huyu mtu yule yule anaanza kuhama katika eneo lake na kuingia mahali asipotakiwa.

Yusufu wa agano la kale alikuwa mjanja sana pale alipoona Mungu yuko pamoja naye na ya kwamba anafanikisha nyumba ya Potifa kwaajili ya mbaraka wa Yususu, haya matokeo mazuri ya kiuchumi ya Yusufu yalipoonekana tu mke wa Potifa aliingiwa na shetani ili alale na Yusufu na hatimaye hatima yake ya mbele ipotee ila huyu kijana alijilinda na hatimaye akafikia ndoto yake. *(Mwanzo 39:1-21)*

Yupo kijana mmoja maandiko yanamsema kuwa mjinga katika *Mithali 7:7-27* huyu hatima yake ilipotea mikononi mwa kahaba ambaye alikuwa amewaangusha wanaume wengi sana kutoka katika Future zao.

## 5.8 ZINAA NI ADUI NAMBA MOJA WA NDOA.

Moja kati ya taasisi ambazo Mungu amehitaji ziheshimiwe ni ndoa, heshima juu ya ndoa ni kitu cha muhimu sana kwamaana imeandikwa ndoa na iheshimiwe na watu wote duniani na malazi yawe safi bali wazinzi na waasherati Mungu atawahukimia adhabu *(Waebrania 13:4)*

Mungu alipomuumba mtu mume alimkusudia atakapoingia katika ndoa awe na mke mmoja tu, hii inamaanisha kumpenda mtu kwaajili ya ndoa ni kuamua kuwaacha wengine kwaajili ya huyo, kwahio hauruhusiwi kutoka nje ya ndoa.

Ukisoma maneno ya Bwana Yesu alisema ndoa hairuhusiwi kuvunjika kwa sababu yeyote ISIPOKUWA KWA UASHERATI, kwahiyo kumbe zinaa ni adui mkubwa wa ndoa anayeweza kusababisha ndoa iachike.

*Mathayo 19:9*

*[9]Nami nawaambia ninyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini.*

## 5.9 ZINAA INARUHUSU MLANGO WA KUPITISHA ROHO CHAFU.

Nimesikia sehemu nyingi wakisema kuwa matumizi ya kondomu yanaweza kukukinga na magonjwa ya zinaa STD [Sexual transmitted Diseases] lakini kondomu haiwezi kukukinga na mapepo ya zinaa STD [Sexual transmitted Demons]

Mtu unayekutana naye katika zinaa unakuwa unashea naye mwili (mnakuwa mwili mmoja) kwahio tegemea kuchota maroho au mikosi kutoka kwake. Na ndiomaana utakuwa shahidi kuwa wachumba wowote wanapokuwa wameanza kushiriki zinaa huwa maisha yao yanabadilika na kuanza kwenda isivyostahili.

*1 Wakorintho 6:16*

*[16]Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja.*

## 5.10 ZINAA HUMUONDOA ROHO MTAKATIFU NDANI YA MTU

Roho Mtakatifu ni Mungu na maandiko yanasema kuwa huyu Roho Mtakatifu anaishi ndani ya watu katika miili yao. Kwahio mwili wa mtu ni hekalu ambalo ndani yake Roho Mtakatifu anaishi.

Sasa zinaa ndio dhambi pekee ambayo maandiko yanasema inatendeka juu ya mwili. Kwahio Roho Mtakatifu hawezi kuishi katika nyumba

iliyoharibiwa kwa zinaa, Zinaa inamuondoa Roho Mtakatifu.

*1 Wakorintho 6:18-19*

*[18]Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.*

*[19]Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe;*

## 5.11 ZINAA INAHARIBU MACHO YA ROHONI.

Moja kati ya hasara za zinaa zinazoleta madhara makubwa hasa kwa mtu wa Mungu ni kutembea katika UPOFU WA KIROHO, jicho la mtu likiwa chafu kwa anayotazama mfano kutazama picha na video chafu, kutazama watu kwa tamaa za mwili na macho humfanya mtu aanze kuharibikiwa uwezo wake wa KUONA mambo ya rohoni.

Wakati utakapoingia katika mambo ya uzinzi na uasherati utashuhudia kutokuona chochote, MAONO huwa yanakata na hata kama ulikuwaga unaota ndoto za maana utashitukia tu zimeisha kwasababu ya zinaa.

Utahangaika kutafuta ishara yeyote rohoni na hautapata kama maandiko yasemavyo;

*Mathayo 16:4*

*[4]Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara; wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona. Akawaacha, akaenda zake.*

## 5.12 ZINAA INALETA HATIA, HOFU NA UCHUNGU.

Hakuna kitu kibaya duniani kama mtu kuishi na hatia, hofu na uchungu. Haya yote matatu ndio vyanzo vikubwa vya matatizo, maisha ya mtu huwa yanabadilika na kuanza kuharibika pale anaporuhusu hofu, hatia na uchungu ndani yake.

Hofu inaweza kumharibia mtu kazi au biashara aliyonayo, hatia inaweza kuharibu ndoa ya mtu, hatia itakufanya ukose ujasiri katika dunia yako.

Zinaa ni dhambi hatari sana kwani ikishafanyika hata kama ni kwa dakika 5 tu huwa inaacha HATIA, UCHUNGU na HOFU ndani ya mtu. Hata kama umeshaiua dhamiri yako bado kuna wakati utafika utahukumiwa tu.

## 6.0 NATOKAJE SASA KWENYE ZINAA?

Maisha ya watu walioanguka katika zinaa huwa yanabaki ya vilio tu vya sirini kama Daudi baada ya uzinzi wake.

Sio mapenzi ya Mungu mtu kuishi katika zinaa kwasababu yeye anataka kila mtu awe katika utakatifu na mwisho aende mbinguni, hii ndiomaana Yesu Kristo alimuonea huruma yule mwanamke mzinzi waliotaka kumponda mawe na baada ya kuwa amemsaidia alimwambia aende zake na asitende dhambi tena.

### •KUHUSU KUTENGA WAZINZI MAKANISANI.

Ni sahihi kuwatenga wazinzi kanisani japo sio vizuri sana kwani wengi wao mnaweza kukuta

hawasaidiki kwa lolote bali mioyo yao inazidi kuharibika kwa kuabishwa na kubaki na hatia isiyoisha ndani yao. Hawa ni watu ambao wanatakiwa kupewa msaada mkubwa zaidi wa kubadilika kuliko kuwatenga kwasababu wengi wanaotengwa huwa wanafikia hatua mtu anaona abaki tu nyumbani na bora afuatilie ibada za mitandaoni. Tukemee zinaa na tuwabaini wenye dhambi ila tusiishie kuwaanika mbele za umati bali tuwaite kwa siri tuwaonye na tuwape darasa binafsi la kuifikia toba ya kweli.

Kwanza mimi ninachoamini hata hawa watumishi ambao wanatenga watu makanisani ndio wa kwanza kwenye dhambi za sirini, wanafananishwa na wale watu waliotaka kumponda mawe mwanamke mzinzi.

*2 Petro 3:9*

*[9]Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*

Zipo mbingu kadhaa ambazo nimekuainishia hapa chini zitakazokusaidia kuishinda zinaa jumla.

## 6.1 KUJIKABIDHI KWA MTUMISHI WA MUNGU.

Zinaa sio dhambi ya kuishinda kimya kimya, kama tabia za zinaa zinakusumbua hatua ya kwanza kuchukua ni kujikabidhi kwa mtumishi wa Mungu mwenye neema ya kumfungua mtu wa aina hii.

Mweleze kila kitu unachopitia yaweza kuwa ni tamaa kali za zinaa, punyeto, kuangalia picha za uchi, ushoga au usagaji.

Ikibidi unaweza ukatoa sadaka yako kuonyesha kiu yako ya kutoka kwenye janga hili japo hatutoi huduma kwa fedha na hautaombwa pesa ila wewe mwenyewe unaweza kuonyesha nia yako kubwa kwa kutoa sadaka ambayo itasimama kama agano, kama ambavyo watu wakuu katika katika biblia wamekuwa wakifanya, mfano ni Nuhu ambaye baada ya kutoa sadaka zake Mungu aliweka upinde wa mvua kama agano la kutokunyesha tena mvua za gharika.

## 6.2 MAOMBI NA KUFUNGULIWA.

•Katika sehemu ya 3 tulijifunza juu ya roho za zinaa kama kisababishi cha dhambi za zinaa, mtu yeyote anayezini kwa vitendo huwa haanzi tu kuzini kwa vitendo lakini ndani yake kunakuwa tayari kuna roho ya zinaa imemuingia na inamfanya azini.

•Wapo watu ambao wamefungwa na roho za uzinzi na tamaa kali, lakini pia wapo ambao katika koo zao wamekuwa wakisumbuliwa na roho za uzinzi, unakuta ni watu wenye ndoa za nje, kutoa mimba na mengine kama hayo.

•Lakini pia yupo ambaye amepata hizi roho za zinaa (majini mahaba) kupitia njia ya kutazama picha za uchi na kujichua, pia kulala na makahaba au watu wenye roho chafu za zinaa.

•Kwa mtu yeyote ambaye anahitaji kutoka katika vifungo hivyo ni muhimu kwanza aombewe na mtu mwenye neema hiyo ili kufunguliwa kutoka kwenye nguvu hizo.  (Unaweza ukanipigia simu kwa namba yangu hapo chini nitakuombea bure na utafunguliwa)..... Hata kama wewe ni mtumishi wa Mungu ila unasumbuka na zinaa nitafute nitakusaidia kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

•Kuombewa ni hatua ya ushindi, mtu akishaombewa inabidi sasa afuate kanuni zingine ili kubadili tabia iliyojengeka kwenye nafsi kwani zinaa sio tu roho ila ni tabia ambayo hujijenga ndani ya mtu,

## 6.3 KUISHI KWA RATIBA.

Imeandikwa kuwa 'pasipo maono watu huacha kujizuia' *(Mithali 29:18)*, hii ni siri kubwa ambayo imewasaidia watu wengi sana kutoka katika vifungo vya uzinzi. Ukishaombewa na ukafunguliwa inabidi uanze kujiingiza katika mfumo wa ratiba ya siku kwa siku ili utengeneze mfumo mwingine wa kimaisha kwani pasipo ratiba/msomo huwezi kujizuia kuzini.

Katika ratiba yako usisahau mambo yafuatayo;

**•Ratiba ya mifungo na maombi.**

Maombi na mifungo ni njia ambayo inamsaidia mtu kuushinda mwili wake, mwili ubapounyima

chakula katika mifungo mirefu mingi na kuutiisha katika mambi huwa unakubali kuishi bila zinaa.

Katika maombi haya pia ni vizuri kuwa ubafanya maombi ya ukiri ambayo nimekuanishia mfano wake hapa chini;

**SENTENSI 40 ZA UKIRI ILI KUTOKA KATIKA NGUVU ZA ZINAA.**

Fanya maombi haya ya ukiri ukitenga walau nusu saa kila siku.  Unaweza kuchagua wakati wa usiku au mapema alfajiri.

Maneno huwa yanafutwa na maneno.

Kama kuna maneno ambao yalitamkwa kwako au yaliandikwa kwenye madhabahu za giza

kukuharibu katika zinaa basi yanatenguliwa kwa maneno yako ya kutengua.

*Isaya 54:17*

*[17]......kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa.......*

Baba katika jina la Yesu Kristo, ninasogea mbele zako kwa nguvu za Roho Mtakatifu na kwa damu ya Yesu Kristo.

1.Mimi sitaitwa mzinzi wala muasherati, nitakuwa msafi mbele zako siku zote.

2.Mimi nitasimama kupinga uzinzi, sitaruhusu uzinzi na uasherati utamkwe kwangu.

3.Mke/mme wangu hatokuwa mzinzi na wala hatatoka nje ya ndoa yetu.

4.Watoto wangu hawataanguka katika zinaa na uasherati.

5.Kanisa langu halitakuwa kanisa la zinaa na uasherati.

6.Kila watu nitakaowazaa kiimani hawatazama katika zinaa na uasherati.

7.Waalimu na wachungaji waniongozao hawataanguka katika uzinzi na uasherati.

8.Bwana Yesu mwili wangu nautoa kama dhabihu kwako, nafsi yangu pia itakutumikia.

9.Macho yangu hayatatazama kwa tamaa za uzinzi.

10.Macho yangu hayataangalia uchi wa mtu na kutamani.

11.Macho yangu hayatavutwa na picha/video za uchi, sitaziangalia kabisa.

12.Ninakataa kutazama uchafu wowote utakaonivuta katika zinaa.

13.Masikio yangu hayatasikiliza maudhui ya kingono.

14.Masikio yangu sitayatega kwenye mazungumzo mabaya.

15.Mikono yangu itakuwa safi, sitaitumia kushika mwili wa asiye mke/mme wangu.

16.Mikono yangu haitatumika kujichua.

17.Miguu yangu sitaipeleka kwa watu wenye midomo michafu.

18.Miguu hangu haitakanyaga hema za wasemao matusi na maneno ya kingono.

19. (Kama ni bikra)...... Bikra yangu sitampa asiye mme/mke wangu, nitajilinda hadi ndoa.

20. (Sio bikra)...... Sitamvulia mtu nguo asiye mme/mke wangu.

21.Sitaingia chumba cha mtu kwaajili ya zinaa na uasherati wake.

22.Sitapokea pesa kwa mtu ambazo badae zitanipelekea kutoa penzi kwake.

23.Sitamhonga mwanaume/mwanamke kwa makusudio ya kulala naye.

24.Sitakula vyakula vilivyotegwa katika kuniangusha kwenye zinaa.

25.Sitavaa nguo zinazoshawishi uzinzi.

26.Sitaongea sauti za kimahaba kwa watu/mtu ambaye sio mwenza wangu.

27.Siwezi kutoa penzi kwa kiongozi wangu kwa kuogopa cheo chake.

28.Siwezi kubaka na haitotokea mimi nikababakwa.

29.Sitatoa mimba wala kushawishi utoaji mimba.

30.Sitatumia njia za uzazi wa mpango mfano kondomu, vijiti, vitanzi au sindano kwa lengo la kuendeleza uzinzi.

31.Sitazungumza na mchumba wangu maneno yanayopelekea kuzini.

32.Siwezi kumtamani mtu wa jinsia yangu.

33.Sitalala na mtu wa jinsia yangu.

34.Ninakataa na kupinga ndoa za jinsia moja.

35.Hakuna mizimu itakayonivuta kwenye zinaa au ndoa za wapenzi wengi na kuchepuka.

36.Hakuna majini mahaba yatakayoniendesha katika uzinzi.

37.Nakataa ndoto zote za mapenzi na ndoa za ndotoni.

38.Mimi nimeshinda zinaa, mimi ni mshindi.

39.Naichukia zinaa na naiona kama mavi.

40.Imekuwa katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai.

**•Ratiba ya kusoma Neno la Mungu, mafundisho na vitabu vya watumishi.**

Dhambi huwa inapoteza nguvu mbele ya maarifa ya neno la Mungu. Ukijizoesha kujaza neno la Mungu ndani yako kutoka kwenye maarifa tofauti tofauti basi utazishinda dhambi za zinaa kwa upesi sana.

*Zaburi 119:11*

*[11]Moyoni mwangu nimeliweka neno lako,*

*Nisije nikakutenda dhambi.*

Kama utahitaji usimamizi wa namna ya kuziweka ratiba hizi vizuri pia nitakushika mkono na baada ya miezi mitatu utakuwa umeshageuzwa na kuwa mtu mwingine.

## 6.4 JITENGE NA VIVUTIO VYA ZINAA.

Pamoja na kuwa na ratiba ya siku kwa siku ila ni lazima mtu anayehitaji ushindi dhidi ya uzinzi ajiepushe na mambo yafuatayo bila kujihurumia kwani imeandikwa ni bora kwenda mbinguni una jicho moja kuliko mwili mzima katika jehamu ***(Mathayo 5:29).***

•Epuka kutazama vichochea uzinzi.

(Video & picha za uchi, movie na miziki ya ngono)

•Epuka kusikiliza mazungumzo mabaya/similizi za mahaba.

•Epuka makundi au watu wabaya.

# 7.0 JINSI NILIVYOZISHINDA DHAMBI ZA ZINAA.

**(Ushuhuda wangu wa kujenga)**

Kabla sijaokoka nilikuwa naishi maisha ya uasherati,

Nilikuwa natazama picha na video za uchi, najichua (punyeto), Nilikuwa siwezi kupitisha wiki sijazini walau mara tatu na zaidi, niliwahi hadi kufukuzwa shule na kufutwa uongozi kisa mahusiano.

Nilipookolewa na Bwana Yesu kupitia mtumishi wake Baba yangu wa kiroho Bish Dickson Cornel Kabigumila nilianza kutafuta namna ambavyo nitaishinda zinaa jumla.

Baada ya kujikabidhi kwa mtumishi wa Mungu na kusema yanayonisumbua  na kuombewa, baadaye niligundua kuwa maombi pekeyake hayatoshi kuniweka huru kwasababu tayari roho za zinaa zimeshaniachia ila bado zinaa imeshakuwa tabia ya kimwili  ndipo nilipojiweka chini ya mafundisho nikapata kanuni kadhaa ambazo ziliwasaidia watu wengine namimi nikaziweka katika matendo.

Niliamua sasa kuanzisha mpango mkakati wa kwangu binafsi ili kuishinda dhambi hio, (Namaanisha nisizini kabisa hata kwa kutamani)

HAYA NDIYO NILIYOANZA KUFANYA KWA MWENDELEZO.

(i)Nilidhamilia kutoka ndani nikaweka agano kwa watu wa juu yangu kuwa sitatazama tena picha

za uchi na kujichua. Pia nilisema hakuna kuyatazama maumbile ya mwanamke zaidi ya mara moja  "jicho la pili/tatu huwa ni la kizinzi"

(ii)Pili nilitengana na marafiki wote wabaya ambao wangeweza kunirudisha dhambini kwa maongezi yao na hata post zao, nilifuta namba nikaanza upya. Pia nilijiondoa kwenye magrup yasiyokuwa na umuhimu mitandaoni, nikafuta 'applications' zilizokuwa zinanishawishi kutazama  na kisikiliza mambo machafu.

(iii)Nilidhamilia pia kutokupost ujinga au masihara kama nilivyokuwa mwanzo. Pia nilisema hakuna kuangalia status za watu ambao hawajielewi,  'nafikili unaelewa...'

(iv)Nilijiwekea ratiba za mifungo mirefu mingi mingi sana ili niushinde na kuuweza mwili,

mifungo ya siku 40 za masaa 12 kwa mizunguko 3 au zaidi kwa mwaka, pamoja na hii ya 3 hadi 5 kavu, na pia nikaanza kuweka ratiba ya kusoma neno walau aya tatu kila siku, nikaweka ratiba ya kusoma vitabu na kusikiliza mafundisho ya watumishi wa Mungu kila siku (wakati mwingine nakesha mikesha binafsi hadi asubuhi)

(v)Pia nilisema hakuna kuangalia Movie na miziki inayochochea zinaa, uraibu wa kucheza magemu na kukaa kwenye makundi ya watu mitaani...hadi niliacha kabisa kuangalia 'TV' ovyo ovyo.

(vi)Nilijiwekea viwango vya maombi ya kunena kwa lugha kila siku na nikadhamilia hakuna kupitisha siku sijaomba walau lisaa limoja na nusu na nusu [nusu saa asubuhi,mchana na jioni]

(vii)Nilidhamilia kutoingia katika mahusiano na mtu zaidi ya mmoja, nikafanya mbinu zote ili nimpate mtu sahihi ambaye nitaingia naye kwenye ndoa bila uzinzi.

**MAOMBI/UKIRI.**

(i)Maombi ya ujazo wa Roho Mtakatifu.

(ii)Mwambie Roho Mtakatifu ahuishe mwili wako *(Warumi 8:11,26)*

(iii)Omba neema ya kuenenda kwa Roho *(Wagalatia 5:25)*

(iv)Omba neema ya kuomba kwa bidii *(Zekaria 12:10)*

(v)Ombea kiu ya neno *(Zaburi 119:11)*

# KUHUSU MTUNZI WA KITABU.

Mimi Dr.Charles Kabigumila ni mtoto wa kiroho wa Ask.Dickson Cornel Kabigumila na ninatumika kama mchungaji msaidizi (2024) chini ya kanisa lake ABC Global Mwanza.

Mimi ni muanzilishi wa huduma inayoitwa DIVINE FAMILY ambayo inawasaidia vijana kwa kuwafundisha kanuni mbali mbali zinazotawala uchumba mfano maisha matakatifu na ushindi dhidi ya zinaa na hatimaye wafikie makusudi yao na kuwa na familia zenye kumtumikia Mungu (Yoshua 24:15).

Mimi ni mwandishi wa vitabu na mpaka sasa nimeandika vitabu 4:-

•Inawezekana kuwa mtakatifu. (Kinauzwa)

•Mke wa mtumishi (Riwaya- inauzwa)

•Moyo wa Ibada. (Bure)

•Vita yangu na kijiji (Bure)

•Mahusiano bila kuchepuka (Kinauzwa)

**By.Pst.Charles Kabigumila tb**

**0746192605**

# KUHUSU KITABU

Kitabu hiki sio tu kitabu bali ni mkusanyiko wa siri ambazo mtu yeyote bila kujali mtumishi wa Mungu au lah, kama akiamua kuziishi basi zitampa maisha mapya ya ushindi dhidi ya dhambi za zinaa. Hiki kizazi tulichopo zinaa imeshika kasi ya ajabu katika ukuaji, miaka elfu 2 iliyopita Bwana Yesu alikiita kile kuwa ni kizazi cha uzinzi sasa unaweza ukafikilia vipi kuhusu sasahivi ambapo wamekuongezea vitu kama video za ngono laivu kwenye simu yako, kwahio kitabu hiki ni muhimu sana katika kizazi hiki na ninakuahidi ushindi mkubwa. Amina.



# KUHUSU MWANDISHI

Dr.Charles Kabigumila ni mtumishi wa Mungu na mwandishi wa vitabu. Ni muanzilishi wa huduma ya Divine Family inayojikita katika kuelimisha vijana juu ya ushindi dhidi ya dhambi hasa za zinaa, inawapa kanuni bora za uchumba na ndoa na mwisho waishi maisha yao ya kusudi.